Cancer Screening in Queensland

Uchunguzi wa saratani (kansa) unaokoa maisha! Uchunguzi hutumia vipimo rahisi kuangalia uwepo wa saratani au hali zinazoweza kupelekea kupata saratani. Vipimo hivi ni muhimu kwa sababu vinaweza kugundua saratani kabla hujaweza kuona au kuhisi mabadiliko yoyote katika mwili wako. Kugundua saratani mapema huwezesha matokeo ya ugonjwa kuwa bora na kuongeza uwezekano wa matibabu kufaulu. Ukiona mabadiliko yoyote katika mwili wako, ni vyema kuongea na daktari wako.

Uchunguzi wa utumbo

Jinsi uchunguzi unavyofanyika

- Kipimo hutafuta uwepo wa damu kwenye kinyesi ambayo ndio njia bora zaidi ya kugundua saratani ya utumbo mapema
- Watu wa umri wa miaka 50-74 hutumiwa **bila malipo kifaa cha kupima baada ya kila miaka miwili** (wenye kadi ya Medicare ya rangi ya kijani kibichi)
- Unaweza pia kumuomba daktari wako kifaa cha kupimia ukiwa umetimia miaka 45

Utafanya nini?

- Kifaa hicho kinapowasili katika sanduku lako la barua, kitumie vile invyostahili
- Ongea na daktari wako kama utakuwa na hofu yoyote

NATIONAL BOWEL CANCER SCREENING PROGRAM

Kwa maelezo zaidi
Piga simu kwa 1800 627 701 au 13 14 50 ili uongee na mfasiri au tembelea mtandao wa health.gov.au/nbcsp

Uchunguzi wa mlango wa kizazi

Jinsi uchunguzi unavyofanyika

- Uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi hutafuta uwepo wa virusi vya HPV (Human Papillomavirus)
- Watu walio na mlango wa kizazi, wanaoshiriki ngono na walio na umri wa miaka 25-74 **wanatakiwa wapime kila baada ya miaka mitano**
- Daktari, muuguzi au wewe mwenyewe waweza kutumia kifaa kilicho zungushiwa pamba kusugua mlango wa kizazi ili kutoa sampuli ndogo

Utahitajika kufanya nini?

- Panga na daktari au muuguzi tarehe ya kufanyiwa kipimo
- Madaktari wengine hutoa huduma hii bila malipo, unaweza kuuliza kama utahitajika kulipia kipimo wakati ukipanga tarehe ya kuenda kwa kipimo
- Unaweza kuomba kufanyiwa kipimo na mhudumu wa afya mwanamke

NATIONAL CERVICAL SCREENING PROGRAM
A joint Australian, State and Territory Government Program

Kwa maelezo zaidi
Piga simu kwa 1800 627 701 au 13 14 50 ili uongee na mkalimani au tembelea mtandao wa health.gov.au/ncsp

eccq Ethnic Communities Council of Queensland

Uchunguzi wa matiti

Jinsi uchunguzi unavyofanyika

- Picha (au ‘x-ray’) ya matiti inayoitwa ‘mammogram’ hutafuta saratani ambazo bado ni ndogo na hazijaweza kuonekana au kugusika
- **Hufanywa bila malipo kwa wanawake wa umri wa miaka 50 na zaidi hapa QLD** (wenye kadi ya Medicare ya rangi ya kijani kibichi).
- Wanawake wenye umri wa miaka 40 pia wanaweza kuomba kufanya uchunguzi
- **Ni muhimu kufanya uchunguzi baada ya kila miaka miwili**

Utafanya nini?

- Kupanga tarehe ya kuenda uchunguzi, piga simu 13 20 50 au 1800 512 451 ili uongee na mfasiri au tembelea mtandao wa www.breastscreen.qld.gov.au
- **Huhitaji rufaa kutoka kwa daktari** ili kufanyiwa uchunguzi wa matiti

BreastScreen Queensland

Kwa maelezo zaidi
Tembelea mtandao wa breastscreen.qld.gov.au

Lung Screening

Jinsi uchunguzi unavyofanyika

- Utapigwa picha ya CT scan yenye miale ya kiwango kidogo kwa kifua chako ili kuangalia dalili za saratani ya mapafu
- Watu wa umri wa miaka kati ya 50-70, wasiokuwa na dalili zozote, ambao kwa sasa wanavuta sigara au waliwacha kuvuta sigara ndani ya miaka 10 iliyopita, na walio na historia ya kuvuta sigara kwa kiwango kinacholingana na miaka ya pakiti 30
- Ikiwa unastahili uchunguzi, unaweza kupimwa **bila malipo baada ya kila miaka miwili**

Utafanya nini?

- Ongea na daktari ili ujue kama unastahili uchunguzi

NATIONAL LUNG CANCER SCREENING PROGRAM

Kwa maelezo zaidi
Piga simu kwa 1800 627 701 au 13 14 50 ili uongee na mfasiri au tembelea mtandao wa health.gov.au/nlcsp

Uchunguzi wa ngozi

Jinsi uchunguzi unavyofanyika

- Kwa sasa hakuna mpango rasmi wa uchunguzi wa saratani ya ngozi hapa Australia

Utafanya nini?

- Fuata kanuni-busara 5 za kujikinga na miale ya jua zinazotolewa na Cancer Council za **Slip, Slop, Slap, Seek, Slide**
- **Chunguza ngozi yako mara** kwa mara kuangalia kama kuna madoa yoyote mapya au mabadiliko katika ukubwa, umbo au rangi ya uvimbe au madoa ambayo umekuwa nayo
- Ongea na daktari wako ukiwa na hofu yoyote na uulize kuhusu uchunguzi wa ngozi

Cancer Council Queensland

Kwa maelezo zaidi
Piga simu 13 11 20 au tembelea mtandao wa cancerqld.org

Proudly supported by

Queensland Government